JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA KILIMO

SHIRIKA LA UKAGUZI NA USIMAMIZI WA VYAMA VYA USHIRIKA
(COASCO)

# TAARIFA HURU YA MKAGUZI NA TAARIFA ZA FEDHA ZA CHAMA KIKUU CHA USHIRIKA WA WA WAKULIMA MARA (WAMACU) LTD KWA MWAKA ULIOISHIA TAREHE 31.03.2022.

Co-operative Audit and Supervision Corporation
(COASCO)
Hatibu Avenue
P.O.Box 761
Telephone:
General line (026) 2323265, 2321485
Director General (026) 2321704
Director of Audit (026) 2322050
Director of Finance and Administration (026) 2321605
Director of Research and Consultancy (026) 2321671
Fax (026) 2321486
E-mail: info@coasco.go.tz
**DODOMA**
**TANZANIA**

**JANUARI, 2023** *ROA*/WAMACU *LTD/2021/2022*

## YALIYOMO


| NA | MAELEZO | UKURASA |
|---|---|---|
| 1. | MAELEZO YA AWALI | 1 |
| 2. | TAARIFA ZA CHAMA | 2 |
| 3. | TAARIFA YA WAJUMBE WA BODI | 3 - 11 |
| 4. | MAELEZO YA WAJIBU WA BODI | 12 |
| 5. | TAARIFA YA MKAGUZI | 13 - 17 |
| 6. | TAARIFA YA FEDHA | 18 |
| 7. | TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI | 19 |
| 8. | TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI | 20 |
| 9. | TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA | 21 |
| 10 | JEDWALI NA UFAFANUZI WA TAARIFA | 22 - 31 |

MAELEZO YA AWALI

Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika
(COASCO) Tanzania Bara

**(Lilianzishwa kwa kifungu cha 3(1) cha Sheria ya Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika Na.15 ya mwaka 1982)**
Kifungu cha 4(1)(a) cha Sheria ya Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika Na.15 ya mwaka 1982 iliyorekebishwa mwaka 2005 kinaipa COASCO Mamlaka ya kuvikagua Vyama vya Ushirika.

**Dira**
Kuwa kituo cha kipekee cha utoaji huduma bora za ukaguzi na ushauri wa Vyama vya Ushirika katika Mashariki mwa Afrika.

**Dhima**
Daima kuendelea kutoa huduma bora ya ukaguzi na ushauri kuongeza utawala bora kwa wateja.

Miiko inayoongoza Shirika kuelekea kwenye Dira yetu na kusaidia kufanikisha Dhima yetu ni kama ifuatavyo:
(i) Kufuata maadili ya taaluma
(ii) Kuzingatia ubora na utoaji huduma haraka
(iii) Kutopendelea, Ushirikiano na Moyo kwa kufanyakazi pamoja
(iv) Elimumwendo na Uvumbuzi
(v) Kutokuwa na ubaguzi wa kijinsia

**Tunafanya haya kwa:**
- Kuchangia katika Usimamizi bora wa fedha za Umma kwa kuhakikisha kwamba wateja wetu wanawajibika kwa rasilimali walizokabidhiwa;
- Kusaidia kuboresha ubora wa huduma za Umma kwa kusaidia uvumbuzi katika matumizi ya rasilimali za Umma;
- Kutoa ushauri wa kitaalamu kwa wateja wetu juu ya mapungufu yaliyopo katika mifumo ya utendaji;
- Kuwashirikisha wateja wetu katika mchakato na mzunguko wa ukaguzi; na
- Kuwapatia wakaguzi wetu vitendea kazi vya kutosha na vifaa vinavyowafanya wawe huru.

**KAULI MBIU**
Daima Kauli Mbiu yetu ni *"COASCO kwa Ukaguzi na Usimamizi bora wa Ushirika"*

# TAARIFA ZA CHAMA

## 1. WAJUMBE WA BODI

| No. | JINA LA MJUMBE | WADHIFA |
|---|---|---|
| 1. | David M Hechei | Mwenyekiti |
| 2. | Michael J Mugwewa | Makamu Mwenyekiti |
| 3. | Samwel G Marwa | Meneja/Katibu |
| 4. | Momanyi Range | Mjumbe |
| 5. | Samwel C Ysoni | Mjumbe |
| 6. | Elius M Samwel | Mjumbe |
| 7. | James M Makoromu | Mwakilishi |

## 2. OFISI ZA CHAMA

S.L.P 228
TARIME
Tarime Mjini,
Barabara ya Nyamwaga
Karibu na Ofisi za Polisi Kanda Maalum

## 3. BENKI YA WAMACU LTD

NMB- Tawi la Tarime
TCB-Tawi la Tarime

## 4. MKAGUZI

Co- operative Audit and Supervision Corporation
(COASCO)
Hatibu Avenue
S.L.P 761
Fax (026) 2321486
E- Mail: info@coasco.go.tz
**DODOMA**
**TANZANIA**

## TAARIFA YA WENYE DHAMANA KWA MWAKA WA FEDHA ULIOISHIA TAREHE 31.03.2022

Wajumbe wa BODI wanayo furaha kuwasilisha taarifa yao pamoja na maelezo ya Taarifa za fedha kwa mwaka ulioishia tarehe 31, March 2022, ambazo zinaonyesha hali halisi ilivyo ya Chama Kikuu cha Ushirika wa Wakulima wa Mara (WAMACU). Taarifa hii imeandaliwa kwa kuzingatia matakwa ya Viwango vya Utayarishaji wa Taarifa za Fedha vya Tanzania (*TFRS 1 Report of Those Charged with Governance*) vinavyotolewa na Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi Tanzania (NBAA).

### UTANGULIZI

Chama Kikuu cha Ushirika cha Wakulima wa Mkoa wa Mara (WAMACU) LTD kilisajiliwa chini ya sheria Namba 20 ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 2003. Chama kiliandikishwa rasmi katika daftari la Mrajis wa vyama vya Ushirika tarehe 24 Desemba, 2008 nakupewa Hati ya usajili yenye Namba 5573.

### DIRA/MTAZAMO

Dira ya chama kikuuu cha ushirika ya wakulima wa Mara Cooperative Union ni kuwa chama imara na endelevu na kinachokidhi mahitaji ya kiuchumi na kijamii ya wanachama wake.

### DHIMA/MADHUMUNI

Dhima kuu ni kuratibu na kuviunganisha vyama vya msingi ambavyo ni wanachama wa union kwa ajili ya mambo yafuatayo;

- Kukusanya, kuhifadhi, kusindika na kutafuta masoko na kuuza mazao hayo kwenye soko lenye tija;
- Kuratibu zoezi la upatikanaji wa mikopo yenye riba nafuu kwa ajili ya maslahi ya wakulima;
- Kuongeza uwezo wa vyama wanachama katika kutoa huduma zenye tija kwa wakulima; na
- Kuwezesha upatikanaji wa miche ya kahawa kwa ajili ya kuongeza kiwango cha uzalishaji.

### MALENGO MAKUU

Malengo ya msingi ya ushirika yanayojumuisha madhumuni ya chama kikuu cha ushirika katika kuinua na kusitawisha hali ya uchumi na maisha ya wanachama kwa ujumla wake, kwa kufuata misingi ya demokrasio ya kweli, sheria, kanuni na taratibu za Tume ya Maendeleo ya ushirika kwa mujibu wa sheria ya vyama vya ushirika Na. 6 ya mwaka 2013.

## MUUNDO WA UONGOZI

Chombo cha juu cha maamzi katika ushirika ni Mkutano Mkuu, Bodi na menejimenti ikiongozwa na Meneja Mkuu.

## TAARIFA YA WAJIBU WA WAJUMBE WA BODI KUHUSIANA NA TAARIFA ZA FEDHA

Kama inavyotamkwa chini ya masharti ya kifungu cha 124 Ibara ndogo 2 na 3 cha sheria ya Vyama Vya Ushirika ya mwaka 2013, Meneja kwa niaba ya wajumbe wa BODI ana wajibu wa kutayarisha taarifa za fedha ambazo zinaonyesha picha halisi ya hali ya union mpaka mwisho wa mwaka wa fedha na ya ziada na nakisi ya union kwa mwaka huo kwa mujibu wa Masharti ya Chama Sehemu Ya Tano (v) Ibara ya 27; na Sera ya uhasibu na fedha Sehemu Ya Nne (iv) ibara ya 8.1

Wajumbe wa BODI wanadhibitisha kwamba sera za uhasibu zinazofaa zimekuwa zikitumiwa kama kawaida na ipasavyo na maamuzi ya busara na makisio vimetolewa katika kutayarisha taarifa za fedha kwa mwaka ulioishia tarehe 31$^{st}$ March, 2022. Wajumbe wa BODI wanadhibitisha pia kwamba kiwango kinachotumika cha uhasibu, viwango vya utoaji taarifa za Fedha kimataifa (IFRs) na ufafanuzi wake vinavyokubaliwa na Bodi ya Viwango vya uhasibu vya kimataifa (IASB) vimekuwa vikifuatwa japokuwa havijafikiwa na kwamba taarifa za fedha zimekuwa zikitayarishwa kwa misingi inayoendelea.

Wajumbe wa BODI wana wajibu wa kuweka rekodi za uhasibu zinazofaa, ambazo zinaonyesha kwa usahihi wakati wote hali ya fedha ya union. Wana wajibu vilevile wa kulinda rasilimali za ushirika na hivyo kuchukua hatua zinazofaa kuzuia na kugundua udanganyifu, makosa na dosari nyingine. Aidha, Wajumbe wa BODI wana wajibu kuweka mfumo toshelezi wa vidhibiti vya ndani.

## MAENDELEO YA SHUGHULI YA BIASHARA

### Matokeo ya Uendeshaji wa Shughuli

Maendeleo ya shughuli ya utendaji wa WAMACU LTD yanazidi kuimarika, hivyo BODI wameandaa na kujumuisha matokeo ya shughuli za UNION ndani ya mwaka mzima, kuanzia April, 2021 hadi March 2022 kama itakavyo-onekana kwenye hesabu za mapato na matumizi katika hesabu ya mazao. Muhtasari wa mapato, matumizi na ziada/nakisi umeonyeshwa hapa chini kama ifuatavyo:-

- Mauzo ya kahawa 500,590,933
- Gharama za mauzo na matumizi 422,730,741
- Ziada ya wakulima 77,860,192

**Maazimio ya Mkutano Mkuu**

Mkutano Mkuu uliazimia mambo yafuatayo:-

- Kumlipa mkulima malipo ya pili hata kama mwaka huu kahawa ilikuwa kidogo;
- Mapendekezo ya bei ya nyongeza iwe TZS. 200 kwa kila kilo moja; na
- Na hicho kiasi cha fedha kitokane na mkopo utakaochukuliwa kwani fedha iliyokuwa imesalia imeisha kusanya kahawa.

**MAUZO YA KAHAWA SAFI KWA MSIMU WA 2021/2022**

Katika msimu wa 2021/2022, Wakulima wa Mara Cooperative Union (WAMACU) Ltd imeuza kahawa safi katika soko la moja kwa moja (direct export) kama ifuatavyo;

| S/N | BATCH | WW.NO | GRADE | BAG | KGS | PRICE (USD) | AMOUNT (USD) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 1 | 1 | FAQ | 300 | 18,000.00 | 136.00 | 48,960.00 |
| 2 | 2 | 1 | FAQ | 300 | 18,000.00 | 136.00 | 48,960.00 |
| 3 | 3 | 1 | FAQ | 276 | 16,560.00 | 136.00 | 45,043.20 |
| 4 | 4 | 1 | FAQ | 28 | 1,680.00 | 140.00 | 4,704.00 |
| 5 | 5 | 2 | FAQ | 400 | 24,000.00 | 136.00 | 65,280.00 |
| 6 | 6 | 2 | FAQ | 4.48 | 288.00 | 140.00 | 806.40 |
| | **TOTAL** | | | **1,308** | **78,528.00** | | **213,753.60** |

Hadi kufikia tarehe ya 31.03.2022 Chama kilikuwa na jumla ya mauzo ya kahawa baada ya makato ya bodi ya kahawa na mauzo ya nje ya Tshs 496,400,258.90/=.

**Aina ya kahawa tunayolima**

Aina ya kahawa inayolimwa na kustawi hapa mkoani wa Mara ni ARABICA, ila yenye tija ni hii ya chotara ambayo inazalishwa na TaCRI. Vilevile WAMACU LTD haiwakilishi Mkoa wa Mara pekee ila kuna wakulima wetu wako mkoa wa Mwanza-Geita wanaolima ROBUSTA na ARABICA, ambao wako kanda ya juu mashariki.

### Utafiti wa kilimo na masoko ya kahawa.

Baada ya kupata watumishi wenye sifa stahiki tutaendelea kushirikiana na taasisi zinazohusika na kilimo na masoko ya kahawa kwa ajili ya kuimarisha uzalishaji wa kahawa. TaCRI imekuwa mdau mkubwa wa biashara yetu katika kupua wigo wa uzalishaji miche kwa ajili ya wakulima wetu.

Hivyo chama kinaendela na jitihada za kukuza uzalishaji wa miche mingi kupitia vikundi vilivyo chini ya TaCRI na TaCRI yenyewe kwa ajili ya kuhakikisha upatikanaji wa miche ya kahawa unaongezeka.

### UKOMO WA MADENI ULIOIDHINISHWA NA MRAJIS WA VYAMA VYA USHIRIKA

Chama kiliidhinishiwa Ukomo wa Madeni kwa Msimu 2021/2022 kama ifuatavyo:

| Na. | MKOPO TSH | MATUMIZI |
|---|---|---|
| 1 | 2,288,405,142/= | Kukusanyia kahawa |
| 2 | 603,376,250/= | Kuongeza thamani na uzalishaji wa kahawa |
| **JUMLA** | **2,891,781,392** | |

### MKOPO ULIOCHUKULIWA KWA MSIMU WA 2021/2022

Kutokana na hali ya uzalishaji kuonekana kuwa ndogo kwa msimu wa 2021/2022, Chama kiliona ni vema kuchukua fedha kiasi ili kuepuka ongezeko la riba , hivyo mkopo ulichukuliwa kama ifuatavyo:-

| Na. | MKOPO TSH | MATUMIZI |
|---|---|---|
| 1 | 550,000,000/= | Kukusanyia kahawa |
| **JUMLA** | **550,000,000/=** | |

### HUDUMA KWA WANACHAMA WAKE

### Ushauri pamoja na namna ya kuandaa makisio

WAMACU ltd, imekuwa msaada mkubwa kwa wanachama wake ambao ni AMCOS, ikiwa ni kuvisaidia kwenye kushauri na hata namna ya kuandaa makisio yao kabla ya kuyapitisha kwa Afisa ushirika Wilaya na kwa Mrajisi wa Mkoa ili yaidhinishwe.

## Mafunzo ya Elimu ya kahawa

Kutokana na wakulima wetu kuwa na elimu ndogo juu ya umuhimu wa ushirika tumepanga kutumia fungu la elimu kuhakikisha elimu ya ushirika na uzalishaji inamfikia kila mkulima; kwa kuanza tumewapatia mafunzo ya mikataba kwa kupitia shirika la Legal Service Facility (LSF) iliyofadhiliwa na TAYLOR WINCH, pia wakulima wetu walipata mafunzo ya usimamizi na uendeshaji wa shughuli za ushirika kwa kupitia taasisi ya BRITEN iliyoletwa na TADB.

## WATUMISHI WA WAMACU LTD

Hadi tarehe 31 March, 2022 WAMACU LTD ilikuwa na wafanyakazi 3 wa wa mkataba ambao ni:- Meneja Mkuu, Meneja shughuli na biashara, na mlinzi. Hivi karibuni tumechukua wanafunzi kwa vitendo ambao ni Mhasibu Msaidizi na Mkaguzi wa ndani.

Uhusiano kati ya menejimenti na BODI umekuwa mzuri kwa kipindi chote cha bodi hii ya mpito.

Kwa ujumla watumishi tulionao kwa sasa ni kama ifuatavyo:

| NA | JINA | WADHIFA | ELIMU | UTAIFA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Samwel Gisiboye Marwa | Meneja Mkuu | Shahada | Mtanzania |
| 2 | Olais Piniel | Meneja shughuli na Biashara | Shahada | Mtanzania |
| 3 | Mohamed Sakilu | Mhasibu Msaidizi | Shahada | Mtanzania |
| 4 | Bashiru Namchambe | Mkaguzi wa Ndani | Shahada | Mtanzani |
| 5 | Yahaya Ryoba | Mlinzi | Darasa IV | Mtanzania |

## WAJUMBE WA BODI YA WAMACU LTD

Majina ya Wajumbe wa BODI ya mpito waliotumikia chama kikuu cha ushirika katika mwaka 2021/2022 hadi tarehe ya taarifa hii ni kama ifuatavyo: -

| NA | JINA | WADHIFA | UTAIFA |
|---|---|---|---|
| 1 | David Mwita Hechei | Mwenyekiti | Mtanzania |
| 2 | Michael Joseph Mugwewa | Makamu M/kiti | Mtanzania |
| 3 | Momanyi Range | Mjumbe | Mtanzania |
| 4 | Elius Marwa Samwel | Mjumbe | Mtanzania |
| 5 | Samwel Chacha Yasoni | Mjumbe | Mtanzania |
| 6 | Samwel Gisiboye Marwa | Katibu | Mtanzania |

MAFANIKIO KATIKA UTEKELEZAJI KWA MWAKA,

Pamoja na changamoto zilizokuwepo UNION ilifanikiwa kutekeleza malengo yake kama ifuatavyo;

a) Chama kinategemea kulipa malipo ya pili kwa wakulima wote;
b) Kufanikisha mchakato wa urejeshaji wa mali za "Ex-MCU(1984) Ltd", kwa kuzifanyia uthaminishaji wake;
c) Kufanikiwa katika kuelimisha wakulima kwa kutoa semina kupitia wafadhili;
d) Kugawa miche kwa wakulima mbalimbali wa Tarime;
e) Kuongeza samani za ofisi na kuwahudumia wakulima;

CHANGAMOTO ZA USHIRIKA

**Wanunuzi binafsi**

Kampuni ya Coffee Management Service (CMS), imeendelea kununua kahawa kwa baadhi ya vyama vya msingi bila kufuata utaratibu. Hii inakinzana na Sheria na Kanuni za ushirika kwa kuwa hata gharama za mikutano, kupeleka makisio, vitabu, marekebisho ya mizani na mchakato wote wa kupata mkopo wa kukusanyia kahawa kwa vyama hivi unagharamiwa na Chama Kikuu. Hii inatupa wakati mgumu wa kufikia makisio ya tani 1,000 tuliyokisia.

**Ukosefu wa mtaji**

Chama chetu hakina vyanzo vyovyote vya mapato kwa ajili ya kuendesha shughuli zake zaidi ya kutegemea mkopo wa benki. Japo chama hiki kinapata ushuru kutokana na mauzo ya kahawa inayokusanywa kutoka kwa wakulima kupitia kwa AMCOS ambao ni mwanachama wa UNIONI.

**Ukosefu wa maghala ya kuhifadhi kahawa**

Tunalazimika kulipia maghala ya kuhifadhi kahawa safi na maganda kwa kuwa maghala haya yapo chini ya Mufilisi. Maghala haya tunakodisha na kulipa kodi ya shilingi milioni moja na laki nane (1,800,000) kwa miezi mitatu ikiwa ni shilingi laki tatu (300,000/=) kwa kila ghala kwa mwezi mmoja.

Tunaomba maghala haya ambayo awali yalikuwa mali ya ushirika basi yangerudishwa na kuwa chini ya ushirika kama ilivyofanyika kwenye mikoa mingine.

**Ukosefu wa usafiri**

WAMACU Ltd haina gari ya kufuata na kuleta kahawa ya mkulima kutoka kwenye vyama vya msingi, hii inatulazimu kukodisha magari ya watu binafsi

ambayo ni changamoto kufuata na kuleta kahawa ya mkulima kwa wakati muafaka. Tungeomba fedha itakayopitishwa kwa ajili ya usafiri kwa msimu wa 2022/2023 ielekezwe kwenye kununua gari moja lenye uwezo wa kuhudumia shughuli za usafirishaji wa kahawa ya maganda kutoka kwenye vyama vya msingi kuja chama kikuu kwa ajili ya kuchakatwa.

**Uzalishaji mdogo**

Kutokana na wakulima kukata kahawa yao na kuwa na mibuni ya zamani inayozalisha kiasi kidogo cha kahawa imepelekea makusanyo ya chama chetu kushuka kwa kila msimu ukilinganisha na kanda zingine zinazozalisha kahawa. Ili kuongeza uzalishaji, WAMACU Ltd wamesaini mkataba naTaasisi ya utafiti wa kahawa (TaCRI) kwa ujenzi wa vitalu na uzalishaji wa miche.

**Ukosekanaji wa kiwanda cha kuchakata kahawa**

Kiwanda cha Ex-MCU kilichopo kwa sasa baada ya AMIR HAMZA, kuondoa mitambo yake aliyokuwa amewekeza hapa MCU, haitaweza kukoboa kahawa ya WAMACU LTD na badala yake tunapeleka kukobolea Northern Highland (Mara Coffee-zamani).

Hii inaiongezea WAMACU LTD gharama kubwa sana, kwani faida yote kumrudia mwenye kiwanda badala ya Ushirika. Kwa mantiki hiyo, kiwanda cha kahawa Ex-MCU kikabidhiwe kwa WAMACU LTD ili kiboreshwe kwa ajili ya kusaidia katika uongezaji wa thamani wa zao la kahawa.

**Malipo tangulizi ya wakulima**

Wakulima wa kahawa wakati wa maandalizi wapewe fedha tangulizi kulingana na shamba na miche ya kahawa iliyoko shambani, hii itamuwezesha Mkulima kumudu gharama za maisha wakati anaendelea kukusanya kahawa yake kwenye Chama cha Msingi/Kikuu.

**MATARAJIO KWA 2022/2023**

i. Mwaka 2022/2023 chama kitaendelea na jitihada zake za utoaji wa mafunzo kwa wanachama wake ili kufikia utoshelevu na tija katika kilimo cha kisasa.
ii. Kuhakikisha WAMACU LTD inakabidhiwa mali za Ex-MCU iliyo chini ya Mufilisi ili kujiongezea nguvu katika mtaji;
iii. Mstakabali wa WAMACU LTD, ni pamoja na kuendelea kusajili wanachama (AMCOS), mashirika binafsi, na kuhimiza utekelezaji wa mpango wa biashara uliowasilishwa TADB kwa ajili ya CPU ya kukoboa kahawa.

iv. Ushirika utajitahidi kuboresha mpango wa motisha kwa wafanyakazi kwa lengo la kuinua ari yao ya kufanya kazi, kuboresha tija na kuendeleza hali ya watumishi ya kuwajibika kwa ushirika.

v. Kwa kushirikiana na Halmashauri idara ya kilimo, TCDC, wizara inayohusika, vyama vya msingi, chuo kikuu cha ushirika na mafunzo ya biashara moshi katika kuboresha na kuinua kiwango cha kilimo cha kisasa kwa wanachama wetu;

vi. Kuwa na kiwanada cha kukoboa kahawa mbivu katika kila AMCOS na WAMACU kuwa na kiwanda cha kukoboa parchment na dry cherry;

vii. Kusajii SACCOS ya WAMACU Ltd kwa ajili ya kuwawezesha wakulima wanachama na Watumishi wa WAMACU Ltd

viii. kipaumbele kitatolewa katika kuinua kiwango cha uwekezaji katika miradi inayofadhiliwa na union katika ujenzi wa CPU;

ix. Ushirika Utajitahidi kuboresha mahusiano yaliyopo baina ya wateja na wafadhili wetu lengo likiwa ni kupanua wigo wa mapato ya union, kuboresha tija na kuendeleza hali ya watumishi na viongozi wa Bodi kuwajibika;

x. Kwa kushirikiana na wizara inayohusika na vyama vya ushirika na chuo kikuu cha ushirika na mafunzo ya biashara moshi, ushirika utaendelea kuimarisha utekelezaji wake wenye lengo la kuboresha kiwango cha uhasibu katika chama chetu cha ushirika na kuhakikisha kuwa hesabu za mwaka zinawasilishwa kwa wakati kwa ajili ya ukaguzi;

xi. Mipango ya utekelezaji ya union italenga kusimamia vizuri miradi kama ilivyoamuliwa kwenye mpango mkakati wa union wa miaka mitano kuanzia mwaka 2021 hadi 20126.

**MICHANGO YA SIASA NA HISANI**

Michango yenye jumla ya Tshs. 550,000/= ililipwa hisani mbalimbali zilizojitokeza hapa WAMACU LTD.

**WAKAGUZI WA HESABU ZA UNION**

Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO) ndiye Mkaguzi wa WAMACU LTD kwa mujibu wa Kifungu cha 4(1)(a) cha Sheria ya Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika NNa.15 ya mwaka 1982 iliyorekebishwa mwaka 2005 na kwa mujibu wa kifungu cha 55(3) cha Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya mwaka 2013.

**HITIMISHO**

Licha ya changamoto zote zilizotajwa katika taarifa ya mwenyekiti ya 2021/2022; WAMACU LTD, katika mwaka 2021/2022 imepata mafanikio mengi.

Kwa hiyo, ni muhimu kutambua jitihada za wajumbe BODI na menejimenti kwa ujumla wake.

Kwa niaba ya Wajumbe wa Bodi;

..................................... ..........................

MWENYEKITI MENEJA

Tarehe 27/01/2023

WAKULIMA WA MARA COOPERATIVE UNION LTD.
27 JAN 2023
S.L.P 2287, RIME
MARA, TANZANIA

## MAELEZO YA WAJIBU WA BODI

Wajumbe wa Bodi wanayo majukumu ya kisheria kupitia kiwango cha *Uwasilishaji wa Taarifa za fedha cha Tanzania* (TFRS1) pamoja na Kifungu cha 55 (2) cha Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013. Mojawapo ya jukumu hilo ni kuandaa Taarifa za fedha za Chama (Hesabu) kwa mtazamo kuwa zinaonyesha hali halisi ya kifedha kila mwisho wa mwaka wa fedha pamoja na matokeo ya shughuli zake kwa mwaka husika. Jukumu la pili ni kuhakikisha kuwa, kwa-umakini mkubwa wanatunza kumbukumbu na vitabu vya hesabu na kwa muda wowote ule zionyeshe hali halisi ya fedha ya chama. Mwisho, wanalo jukumu la kuhakikisha kuwa mali za chama wanazilinda na kuzitunza na wakati wote zinakuwa katika hali ya usalama.

Wajumbe wa Bodi ndio walio na jukumu au wajibu wa uandaaji na uwasilishaji wa Taarifa hizi za fedha kulingana na Viwango vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha vya Kimataifa (na ambavyo pekee vinakubalika kutumika nchini) pamoja na matakwa ya Sheria ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 2013. Jukumu hili linahusisha: kubuni, kutumia na kulinda mfumo wa uthibiti wa mali ndani ya UNION ambao utakuwa sanjari na uandaaji na uwasilishaji wa taarifa za kifedha zisizo na dosari kubwa pamoja na kuweka mifumo ya kihasibu na jinsi ya kufanya makadirio katika hesabu mbalimbali yaliyo na mantiki kwa wakati huo.

Bodi inakubali jukumu hili na kubainisha kuwa hesabu hizi zimeandaliwa kwa kufuata miongozo ya uhasibu iliyopo sasa kama inavyotolewa na Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi Tanzania (NBAA) na ile ya Kimataifa (IFRS).

Taarifa hii pamoja na hesabu zilizoambatanishwa zimeidhinishwa na Bodi ya UNION tarehe ....27/01/2023.... na kusainiwa kwa niaba ya Bodi na:

| | |
|---|---|
| ................................ | 27/01/2023 |
| MWENYEKITI | TAREHE |
| ................................ | 27/01/2023 |
| MJUMBE | TAREHE |

WAKULIMA WA MARA COOPERATIVE UNION LTD. 27 JAN 2023 S.L.P. 2291, RIME MARA, TANZANIA

# TAARIFA HURU YA MKAGUZI KWA WANACHAMA WA CHAMA KIKUU CHA USHIRIKA WA WAKULIMA WA MARA (WAMACU) LTD

## Ripoti Inayohusu Taarifa za Fedha kwa Mwaka Ulioishia Tarehe 31.03.2022

### *Hati Yenye Shaka*

Tumekagua taarifa za fedha za Kikuu Cha Ushirika Wa Wakulima Wa Mara (WAMACU) Ltd, ambazo zinajumuisha taarifa ya hali ya fedha ya tarehe 31 Machi, 2022, na taarifa ya mapato na matumizi, taarifa ya mabadiliko ya mtaji na taarifa ya mtiririko wa fedha kwa mwaka ulioishia tarehe hiyo, na maelezo ya ufafanuzi wa taarifa za fedha, kujumuisha muhtasari wa sera muhimu za uhasibu.

Kwa maoni yetu, isipokuwa kwa matokeo ya mambo yaliyoelezwa katika aya ya msingi wa hati yenye shaka ya ripoti yetu, taarifa za fedha zilizoambatanishwa zinaonesha hali halisi ya fedha ya Chama cha Ushirika ya tarehe 31 Machi, 2022, na matokeo ya shughuli zake pamoja na mtiririko wa fedha kwa mwaka ulioishia tarehe hiyo kulingana na matakwa ya Viwango vya Kimataifa vya Utoaji Taarifa za Fedha.

### *Msingi wa Hati Yenye Shaka*

1. **Bakaa ya deni la mkopo kutoka benki ya TADB TZS 403,695,386 katika taarifa za fedha za Chama inatofautana na hati ya uthibitisho wa deni kutoka benki ya TADB kwa TZS 199,321,739**

   Wakati wa ukaguzi tulibaini kwamba hati ya uthibitisho wa bakaa ya mkopo kutoka benki ya TADB inaoneshwa chama kudaiwa TZS 603,017,125 wakati taarifa za fedha za chama zikionesha bakaa ya TZS 403,695,386 na hivyo kutofautiana kwa TZS 199,321,739 kunako tarehe 31.03.2022. Hakuna malinganisho yaliyofanyika kati ya chama na benki ya TADB kwa lengo la kufanya masahihisho katika taarifa za fedha za chama. Kwa sababu hiyo hatukuweza kuthibitisha usahihi wa bakaa ya mkopo kutoka benki ya TADB TZS 403,695,386 kama ilivyowasilishwa kwenye taarifa za fedha kunako tarehe 31.03.2022.

2. **Wadai wa TZS 102,047,940 wamefutwa kupitia taarifa ya madabiliko ya mtaji badala ya taarifa ya mapato na matumizi**

   Katika mwaka wa fedha 2021/2022 chama kilipata kibali cha Mrajis kufuta wadai wa TZS 102,047,940 kutoka kwenye taarifa za fedha za chama. Hata hivyo, hesabu hiyo imefutwa kupitia taarifa ya mabadiliko ya mtaji badala ya kutambuliwa kama mapato mengineyo katika taarifa ya mapato na matumizi. Kwa sababu hiyo matokeo ya uendeshaji katika taarifa ya

mapato na matumizi kwa mwaka 2021/2022 yamepotoshwa kwa TZS 102,047,940 ambazo zimeingizwa katika taarifa ya mabadiliko ya mtaji kinyume matakwa ya kiwango cha uhasibu Na.1 kuhusu uwasilishaji taarifa za fedha.

3. **Uwezo wa Chama kuendelea kujiendesha kwa tija katika siku za usoni uko mashakani**

Tathmini yetu ya uwezo wa chama kuendelea kujiendesha kwa tija katika siku za usoni imebaini kuwa vipo viashiria vya kutia shaka juu ya uwezo wa chama kuendelea kujiendesha kwa tija siku za usoni. Baadhi ya mambo tuliofanyia tathmini wakati wa ukaguzi ni kama ifuatavyo:

i) Chama kupata hasara za mara kwa mara ambazo zimesababisha limbikizo la hasara kufikia TZS 394,767,653 hapo tarehe 31.03.2022. Kwa mwaka 2021/2022 pekee chama kimepata hasara ya TZS 120,295,240;
ii) Kushindwa kulipa madeni ya muda mfupi na mrefu
iii) Chama kushindwa kukusanya madeni yake kutoka kwa wadaiwa
iv) Chama kuwa na mtaji hasi kiasi cha TZS 389,057,287

Pamoja na mambo mengine kwa ujumla yanaaashiria uhai wa chama kuwa mashakani kwa siku za usoni. Pamoja na hali hiyo Bodi haikuelezea bayana kuhusu tatizo la uhai wa chama na jinsi inavyojipanga kuondokana na viashiria vinavyofanya uwezo wa chama kujiendesha kwa tija katika siku za usoni kuwa mashakani.

Ukaguzi wetu ulifanyika kwa kuzingatia Viwango vya Ukaguzi vya Kimataifa. Wajibu wetu chini ya hivyo viwango umeelezwa katika aya ya wajibu wa mkaguzi kwa taarifa za fedha ya taarifa yetu. Tuko huru kulingana na matakwa ya maadili yanayohusiana na ukaguzi wetu wa taarifa za fedha Tanzania, na tumetimiza wajibu wetu mwingine wa maadili kulingana na matakwa haya. Tunaamini ushahidi wa ukaguzi ambao tumeupata unatosheleza na unafaa kwa ajili ya msingi wa hati yenye shaka.

### *Masuala Muhimu ya Ukaguzi*

Masuala muhimu ya ukaguzi ni yale kwa ukadirifu wa taaluma yalikuwa muhimu zaidi katika ukaguzi wa taarifa za fedha za mwaka huu. Masuala haya yalielezwa katika muktadha wa ukaguzi wetu wa taarifa za fedha kwa ujumla, na katika kutoa maoni yetu juu yake, hatutoi rnaoni tofauti katika masuala haya.

## Taarifa Nyingine

Uongozi wa Chama unawajibika kwa ajili ya taarifa nyingine. Taarifa nyingine ni pamoja na taarifa ya Wajumbe wa Bodi na Tamko la Mkuu wa Idara ya Fedha lakini hazijumuishi taarifa za fedha na taarifa yetu ya ukaguzi.

Maoni yetu juu ya taarifa za fedha hayahusishi taarifa nyingine na hatutoi uthibitisho wa aina yoyote juu yake. Ukiunganisha na ukaguzi wetu wa taarifa za fedha, wajibu wetu ni kusoma taarifa nyingine na kwa kufanya hivyo, tunaangalia kama taarifa nyingine kwa kiasi kikubwa haziendani na taarifa za fedha au uelewa wetu tulioupata wakati wa ukaguzi, ama vinginevyo zinaonekana kupotoshwa.

Iwapo, kutokana na kazi tuliyoifanya kuhusu taarifa nyingine itabainika kwamba kunaupotoshaji wa taarifa hizi nyingine, tunatakiwa kutoa taarifa juu ya ukweli huo. Hatuna jambo la kutolea taarifa kuhusu suala hili.

### *Wajibu wa Bodi ya Chama cha Ushirika*

Bodi ya Chama cha Ushirika inawajibu wa kutayarisha na kuwasilisha taarifa hizi za fedha kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Utoaji Taarifa za Fedha pamoja na Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya mwaka 2013. Vilevile bodi inawajibu wa kuweka mfumo wa udhibiti wa ndani ambao bodi inaona ni muhimu katika kutayarisha taarifa za fedha ambazo hazina dosari kubwa zinazotokana na udanganyifu au makosa ya kawaida.

Katika kutayarisha taarifa za fedha bodi inawajibu wa kutathmini uwezo wa Chama kuwa endelevu, ikionesha, kadri inavyofaa, mambo yanayohusiana na Chama kuwa endelevu na kutumia msingi wa uhasibu wa Chama kuwa endelevu isipokuwa ama bodi inakusudia kukifilisi Chama au kusitisha shughuli au hakina njia mbadala ya kweli isipokuwa kufanya hivyo.

### *Wajibu wa Mkaguzi*

Shabaha yetu ni kupata uhakika wa maana kama taarifa za fedha kwa ujumla wake hazina upotoshaji mkubwa, ama kwa sababu ya udanganyifu au makosa ya kawaida, na kutoa taarifa ya mkaguzi ambayo inajumuisha maoni yetu. Uhakika wa maana ni kiwango cha juu cha uhakika, lakini siyo dhamana kwamba ukaguzi uliofanyika kulingana na viwango vya ukaguzi vya kimataifa kila mara utagundua upotoshaji mkubwa unaokuwepo. Upotoshaji unaweza kutokana na udaganyifu au makosa ya kawaida na unafikiriwa kuwa mkubwa kama, peke yake au kwa ujumla, ungeweza kuathiri maamuzi ya watumiaji kwa msingi wa taarifa hizi za fedha.

Vilevile, kifungu cha 55(6) cha Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya mwaka 2013 kinatutaka tujiridhishe kama shughuli za Chama cha Ushirika zimefanyika kulingana na matakwa ya Sheria au la na, kama vitabu na hesabu za Chama vina kubaliana na vinatoa hali halisi ya shughuli za Chama.

Kama sehemu ya ukaguzi kulingana na Viwango vya Ukaguzi vya Kimataifa, tunatumia maamuzi ya weledi na tunadumisha weledi wa kushuku wakati wote wa ukaguzi. Pia:

- Tunatambua na kutathmini hatari za upotoshaji mkubwa wa taarifa za fedha, ama kutokana na udanganyifu au makosa ya kawaida, kupanga na kufanya ukaguzi kuitikia hatari hizo, na kupata ushahidi unaotosheleza na kufaa kwa ajili ya msingi wa maoni yetu. Hatari ya kutogundua upotoshaji mkubwa unaotokana na udanganyifu ni kubwa kuliko hatari inayotokana na makosa ya kawaida, kwa sababu udanganyifu unaweza kuhusisha njama, kughushi, kuondoa taarifa kwa makusudi, mawasilisho yasiyo sahihi, au kupuuza mfumo wa udhibiti wa ndani.

- Kupata ufahamu wa udhibiti wa ndani kuhusiana na ukaguzi ili kupanga njia za ukaguzi ambazo zinafaa, lakini siyo kwa makusudi ya kutoa maoni juu ya kufaa kwa udhibiti wa ndani wa Chama.

- Kutathmini kufaa kwa sera za uhasibu zinazotumika na usahihi wa makadirio ya uhasibu na maelezo bayana yaliyofanywa na uongozi.

- Kuhitimisha kufaa kwa matumizi ya bodi juu ya msingi wa uhasibu wa Chama kuwa endelevu na, kwa kuzingatia ushahidi wa ukaguzi uliopatikana, ama kuwepo kwa mashaka makubwa kuhusiana na matukio au hali inayoweza kuleta mashaka makubwa juu ya uwezo wa Chama kuendelea kuwa endelevu. Kama tunahitimisha kwamba yapo mashaka makubwa, tunatakiwa kuvuta nadhari katika taarifa yetu ya ukaguzi kuhusiana na maelezo bayana katika taarifa za fedha au, kama maelezo hayo hayatoshelezi, tubadilishe maoni yetu. Hitimisho letu limejengwa juu ya ushahidi wa ukaguzi tulioupata hadi kufikia tarehe ya taarifa yetu ya ukaguzi. Hata hivyo, matukio au hali za siku za usoni zinaweza kusababisha Chama kukoma kuendelea kuwa endelevu.

Tunawasiliana na Bodi ya Chama cha Ushirika kuhusiana, miongoni mwa mambo mengine, mawanda yaliyopangwa na muda wa ukaguzi na matokeo makubwa ya ukaguzi, kujumuisha mapungufu yoyote makubwa katika udhibiti wa ndani ambayo tunayabaini wakati wa ukaguzi wetu.

Pia tunatoa taarifa kwa Bodi ya Chama cha Ushirika ya kwamba tumefuata matakwa ya miiko ya kuwa huru, na tunawasiliana nao kuhusu mahusiano na mambo mengine yote yanayoweza kufikiriwa kukiuka uhuru wetu na pale inapobidi jinsi ya kuulinda.

**Ripoti Inayohusu Matakwa Mengine ya Kisheria na Usimamizi**

Kulingana na matakwa ya kifungu cha 55(6) cha Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya mwaka 2013, tunatoa taarifa kwa maoni yetu kwamba:

a) Vitabu vya hesabu vilivyotunzwa na Chama vinakubaliana na vinatoa hali halisi ya shughuli za Chama; na

b) Shughuli za Chama zimefanyika kulingana na madhumuni ya Chama, Masharti na maamuzi yaliyofanyika katika mkutano mkuu wa Chama.

**SHIRIKA LA UKAGUZI NA USIMAMIZI WA VYAMA VYA USHIRIKA (COASCO)**

CO-OPERATIVE AUDIT & SUPERVISION CORPORATION
P. O. Box 761
DODOMA

**CPA Z.E. MKINGULE**
**MKURUGENZI MKUU**

**Barabara ya Hatibu**
**DODOMA**

**Tarehe:** 27/01/2023

Nakala: Mrajis wa Vyama vya Ushirika
**DODOMA**

Mrajis Msaidizi wa Vyama vaya Ushirika
**MARA**

## TAARIFA YA MIZANIA KUNAKO TAREHE 31 MACHI 2022

| | | 31.03.2022 TZS | 31.03.2021 TZS |
|---|---|---|---|
| RASILIMALI | NOTE | | |
| Mali ya Kudumu | 2 | 1,998,750 | 1,668,750 |
| Uwekezaji wa Hisa | 3 | 6,000,000 | - |
| Jumla | | 7,998,750 | 1,668,750 |
| | | | |
| Rasilimali za Muda Mfupi | | | |
| Bidhaa ghalani | 4 | 31,128,000 | 7,764,086 |
| Wadaiwa wengine | 5 | 169,021,018 | 172,550,549 |
| Fedha Taslim na Benki | 6 | 41,648,424 | 257,862,313 |
| Jumla ya Rasilimali za muda mfupi | | 241,797,442 | 438,176,948 |
| JUMLA YA RASILIMALI | | 249,796,192 | 439,845,698 |
| | | | |
| MTAJI NA DHIMA | | | |
| Mtaji | | | |
| Akiba za kisheria | 7 | 5,710,366 | 5,710,366 |
| Limbikizo la Hasara | | (394,767,653) | (376,520,353) |
| Jumla ya Mtaji | | (389,057,287) | (370,809,987) |
| | | | |
| Wadai wa muda Mrefu | 8 | 403,695,386 | 440,000,000 |
| | | | |
| Dhima ya Muda Mfupi | | | |
| Hisa za wanachama | | 7,700,000 | 7,700,000 |
| Malipo ya wakulima | 9 | 201,075,455 | 123,215,263 |
| Wadai wengine | 10 | 26,382,639 | 239,740,423 |
| Jumla ya Wadai | | 235,158,094 | 370,655,685 |
| JUMLA YA MTAJI NA DHIMA | | 249,796,192 | 439,845,698 |

JEDWALI NA.1 HADI NA.16 NI SEHEMU YA HESABU HIZI

............................ MWENYEKITI

............................ MENEJA

TAREHE 27/01/2023

## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2021/2022

| | JEDW | 2021/2022 TZS | 2020/2021 TZS |
|---|---|---|---|
| MAPATO | | | |
| Ushuru wa chama kikuu | 11 | 10,626,540 | 17,730,300 |
| Mapato mengine | 12 | 11,478,456 | 5,206,000 |
| Jumla ya Mapato | | 22,104,996 | 22,936,300 |
| | | | |
| TOA; MATUMIZI | | | |
| Gharama za watumishi | 13 | 30,114,050 | 25,988,250 |
| Gharama za utawala | 14 | 112,286,186 | 32,144,993 |
| Jumla ya Matumizi | | 142,400,236 | 58,133,243 |
| Faida/(hasara) ya mwaka | | (120,295,240) | (35,196,943) |

JEDWALI NA.1 HADI NA.16 NI SEHEMU YA HESABU HIZI

..................................... ..........................

MWENYEKITI MENEJA

TAREHE 27/01/2023

## TAARIFA YA MTAJI UZUNGUKAO KUISHIA TAREHE 31ST MARCH 2022

| | MATENGO YA KISHERIA 20% | AKIBA YA KUKOMBOLEA HISA 15% | LIMBIKIZO LA ZIADA/(UPUNGUFU) | JUMLA |
|---|---|---|---|---|
| | TZS | TZS | TZS | TZS |
| Salio mwanzoni 01.04.2020 | 3,263,066 | 2,447,300 | (399,903,410) | (394,193,044) |
| Marekebisho ya hesabu | | | 58,580,000 | 58,580,000 |
| Salio anzia lililorekebishwa | 3,263,066 | 2,447,300 | (341,323,410) | (335,613,044) |
| Ziada(upungufu) wa mwaka | | | (35,196,943) | (35,196,943) |
| Salio mwishoni 31.03.2021 | 3,263,066 | 2,447,300 | (376,520,353) | (370,809,987) |
| | | | | |
| Salio mwishoni 31.04.2021 | 3,263,066 | 2,447,300 | (376,520,353) | (370,809,987) |
| Wadai waliofutwa | | | 102,047,940 | 102,047,940 |
| Ziada(upungufu) wa mwaka | | | (120,295,240) | (120,295,240) |
| Salio mwishoni 31.03.2022 | 3,263,066 | 2,447,300 | (394,767,653) | (389,057,287) |

JEDWALI NA.1 HADI NA.16 NI SEHEMU YA HESABU HIZI

.............................. ..............................

MWENYEKITI MENEJA

TAREHE 27/01/2023

## TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KUISHIA TAREHE 31 MACHI 2022

| | 2021/2022<br>TZS | 2020/2021<br>TZS |
|---|---|---|
| SHUGHULI ZA UENDESHAJI | | |
| Ziada/(upungufu) wa mwaka | (120,295,240) | (35,196,943) |
| Ongeza Uchakavu | 1,800,000 | |
| Ziada/(upungufu) katika hesabu ya mazao | - | - |
| Ziada katika shughuli za uendeshaji | (118,495,240) | (35,196,943) |
| Mtaji uzungukao: | | |
| Punguzo(Ongezeko) la Bidhaa ghalani | (23,363,914) | (564,086) |
| Punguzo(Ongezeko) la wadaiwa | 3,529,531 | (59,955,911) |
| Ongezeko(Punguzo) la wadai | (213,357,784) | 101,970,601 |
| Ziada/(upungufu) katika hesabu ya mazao | 77,860,192 | 83,980,722 |
| Fedha halisi shughuliza uendeshaji | (273,827,215) | 90,234,383 |
| | | |
| SHUGHULI ZA UWEKEZAJI | | |
| Ununuzi wa mali ya Kudumu | (2,130,000) | (1,668,750) |
| Ununuzi wa Hisa KCBL na TFC | (6,000,000) | - |
| Fedha halisi shughuliza uwekezaji | (8,130,000) | (1,668,750) |
| | | |
| SHUGHULIZA MTAJI | | |
| Wadai waliofutwa | 102,047,940 | - |
| Mkopo kutoka TADB | 550,000,000 | - |
| Marejesho ya Mkopo TADB | (586,304,614) | 440,000,000 |
| Fedha halisi shughuli za fedha | 65,743,326 | 440,000,000 |
| | | |
| Fedha halisi iliyoongezeka katika mwaka | (216,213,889) | 528,565,631 |
| Fedha iliyokuwepo mwanzoni mwa mwaka 01.04.2021 | 257,862,313 | (270,703,318) |
| Fedha iliyopo mwishoni mwa mwaka 31.03.2022 | 41,648,424 | 257,862,313 |
| | | |
| Bank NMB PLC (Ofisi Kuu) | 850,104 | 5,338,398 |
| NMB Bank PLC (coffee) 30410006857 | 38,822,838 | 35,402,315 |
| Tanzania Commercial Bank | - | 217,121,600 |
| CRDB Benki (coffee) 0150590775600 | 1,975,482 | - |
| Jumla | 41,648,424 | 257,862,313 |

JEDWALI NA.1 HADI NA.16 NI SEHEMU YA HESABU HIZI

.......................... ..........................

MWENYEKITI MENEJA

TAREHE 27/01/2023

## JEDWALI NA MAELEZO YA UFAFANUZI WA TAARIFA ZA FEDHA KUISHIA TAREHE 31 MACHI 2022

### 1.1 MAELEZO BAYANA

Chama Kikuu cha Ushirika cha Wakulima wa Mkoa wa Mara (WAMACU) LTD kilisajiliwa chini ya sheria Namba 20 ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 2003 (Iliyofanyiwa marekebisho na Sheria Na.6 ya Mwaka 2013). Chama kiliandikishwa rasmi katika daftari la Mrajis wa vyama vya Ushirika tarehe 24 Desemba, 2008 nakupewa Hati ya usajili yenye Namba 5573.

Madhumuni ya chama hiki yanatokana na kifungu cha 24 cha sheria ya Vyama vya Ushirika Na 6 ya mwaka 2013 kama ifuatavyo:

i. Kukusanya, kuhifadhi, kusindika na kutafuta masoko na kuuza mazao hayo kwenye soko lenye tija;
ii. Kuratibu zoezi la upatikanaji wa mikopo yenye riba nafuu kwa ajili ya maslahi ya wakulima;
iii. Kuongeza uwezo wa vyama wanachama katika kutoa huduma zenye tija kwa wakulima; na
iv. Kuwezesha upatikanaji wa miche ya kahawa kwa ajili ya kuongeza kiwango cha uzalishaji.

Makao makuu ya chama hiki yako katika Wilaya ya Tarime, Mkoa wa Mara

### 1.2 MUHTASARI WA KANUNI KUU ZA UHASIBU

Kanuni kuu zilizotumika kuandaa hesabu hizi zimeorodheshwa hapa chini. Kanuni hizi zitaendelea kutumika bila ya mabadiliko mwaka hadi mwaka, isipokuwa pale ambapo itabidi kufanya mabadiliko, maelezo yatatolewa kueleza sababu za mabadiliko hayo.

#### 1.2.1. Msingi wa uandaaji

Taarifa hizi za fedha zimeandaliwa kwa misingi ya viwango vya kimataifa vya utoaji wa Taarifa za Kifedha (IFRS). Taarifa za fedha zimeandaliwa kwa kutumia kumbukumbu za miamala iliyokwisha tendeka huko nyuma, iliyorekebishwa kwa uthaminishwaji wa mali, kwa bei iliyoridhiwa.

Uandaaji wa hizi taarifa za fedha ili zirandane na IFRS inahitaji matumizi ya mabadiliko muhimu ya kihasibu; pia, huhitaji uongozi kufanya maamuzi wakati wa kutumia kanuni za hesabu za chama. Viwango vya Kimataifa vya Utoaji wa Taarifa za fedha vilivyotumika katika kuandaa taarifa hizi ni kama ifuatavyo:

| | |
|---|---|
| IAS 1 | Upangaji wa Taarifa za Kifedha |
| IAS 2 | Bidhaa |
| IAS 7 | Taarifa za Mtiririko wa Fedha |
| IAS 8 | Kanuni za Uhasibu, Mabadiliko katika Makadirio na Makosa ya Uhasibu |
| IAS 16 | Majengo, Mitambo na Zana |
| IAS 24 | Kuweka Bayana Mahusiano na Watu au asasi walio Karibu na viongozi yanayoweza kuleta mgongano wa kimaslahi |
| ISA 37 | Matengo, Madeni na Madai Yamkini |
| IFRS 15 | Utambuzi wa mapato |

### 1.2.2. Mali za Kudumu

1.2.2.1 Thamani ya Mali za Kudumu

Mali za kudumu huthaminiwa kwa kutumia thamani halisi iliyotumika kununua mali hizo. Mali za kudumu zimeonyeshwa katika Taarifa ya hali ya fedha kwa kutumia thamani halisi wakati wa ununuzi wa mali hiyo au uthaminishaji uliofanyika baada ya mali hiyo kutumika kwa muda fulani, baada ya kupunguza malimbikizo ya uchakavu kwa njia nyoofu wa mali hizo.

#### 1.2.2.2 Uchakavu wa Mali

Tengo la Uchakavu wa Mali za Kudumu hutolewa kufuatia gharama za mali, hizo zimedumu kwa kutumia mtindo wa uchakavu mnyoofu kwa asilimia zifuatazo:

| Aina ya **mali** | **Asilimia ya Uchakavu** |
|---|---|
| Kompyuta | 37.5% |
| Viti | 37.5% |
| Turubai | 37.5% |

### 1.2.3 Bidhaa

Bidhaa mwishoni huthaminishwa kwa kutumia gharama halisi zilizotumika katika ununuzi wa bidhaa hiyo pamoja na gharama za uchukuzi, usogezaji na utunzaji katika ghala hiyo. Tengo kwa ajili ya bidhaa iliyomaliza muda wake wa kutumika na iliyoharibika kabla ya kumaliza muda wake huwekwa kwa 100%.

### 1.2.4 Matengo ya Kisheria

Kifungu cha 67 cha Kanuni za Vyama Vya Ushirika ya 2015 inaelekeza jinsi ya Kugawanya ziada ya mwaka kama ifuatavyo:

(a) Akiba ya lazima isipungue 20% ya ziada iliyopatikana kwa mwaka

(b) Akiba ya kukombolea Mafungu isizidi 15% ya ziada ya mwaka na isizidi 15% ya mtaji mkuu wa chama ambao hujumuisha mafungu ya mwanachama, akiba ya lazima na mtaji utokanao na michango kutoka kwa asasi na wadau wengine. Akiba hii itatumika katika kulipia mafungu ya wanachama ambao wamejitoa uanachama wenyewe au waliovuliwa uanachama

**Jedwali Na.2 Mali ya Kudumu**

| **Mwaka 2022** | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Kompyuta ya Mezani | Printa | Viti na Meza | Turubai | Jumla |
| Maelezo | TZS | TZS | TZS | TZS | TZS |
| Thamani ya kununulia | 1,300,000 | 500,000 | 620,000 | 250,000 | 2,670,000 |
| Ongezeko | | | 2,130,000 | | 2,130,000 |
| Jumla (cost) 31/03/2022 | 1,300,000 | 500,000 | 2,750,000 | 250,000 | 4,800,000 |
| Uchakavu: (%) | 37.50 | 37.50 | 37.50 | 37.50 | |
| | | | | | |
| Uchakavu mwanzoni | 487,500 | 187,500 | 232,500 | 93,750 | 1,001,250 |
| Uchakavu mwaka huu | 487,500 | 187,500 | 1,031,250 | 93,750 | 1,800,000 |
| Jumla | 975,000 | 375,000 | 1,263,750 | 187,500 | 2,801,250 |
| Baki vitabuni 31/03/2022 | 325,000 | 125,000 | 1,486,250 | 62,500 | 1,998,750 |

| Jedwali za Taarifa za fedha kuishia tarehe 31 machi 2022 | | | |
|---|---|---|---|
| | | 31.03.2022<br>TZS | 31.03.2021<br>TZS |
| Jedwali Na.3 | **Uwekezaji wa Hisa** | | |
| | Hisa KCBL | 5,000,000 | - |
| | Hisa TCF | 1,000,000 | - |
| | Jumla | 6,000,000 | - |
| | | | |
| Jedwali Na.4 | Bidhaa ghalani | | |
| | *Kahawa safi (Kgs 7,782*4,000/=) | 31,128,000 | 7,764,086 |
| | *Kahawa iliyobanguliwa | | |
| | | | |
| Jedwali Na.5 | Wadaiwa wengine | | |
| | Vyama vya Msingi mbalimbali | 5,824,680 | 5,824,679 |
| | Muriba AMCOS | 4,266,867 | 184,467 |
| | Bungurere AMCOS | 24,901,224 | 27,730,200 |
| | Gorong'a AMCOS | 3,904,820 | 10,247,500 |
| | Nyantira AMCOS | 3,041,881 | 3,041,881 |
| | Maisome AMCOS | 286,246 | 286,246 |
| | Tagare AMCOS | 1,723,850 | - |
| | Kema AMCOS | 5,201,200 | - |
| | Kangariani AMCOS | 137,310 | - |
| | Mbogi AMCOS | 7,797,900 | - |
| | Itiryo AMCOS | 1,993,020 | - |
| | Nyakonga AMCOS | 1,193,020 | - |
| | Nyandurumo AMCOS | 565,840 | - |
| | Kemakorere AMCOS | 1,068,800 | - |
| | Nyamwigoma AMCOS | 514,500 | - |
| | Mogabiri AMCOS | 313,200 | - |
| | Nkongore AMCOS | 379,100 | - |
| | Jumla ndogo | 63,113,458 | 47,314,973 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Jedwali Na.5 | *(jedwali linaendelea...)* | **31.03.2022 TZS** | **31.03.2021 TZS** |
| | Mwesu AMCOS | 502,440 | - |
| | Shadabi AMCOS | 1,000,000 | - |
| | Mkopo Watumishi | 17,960,000 | - |
| | Tarime DC | 4,810,016 | 4,810,016 |
| | Tarime TC | 425,560 | 425,560 |
| | Malipo ya awali TACRI (vitalu vya kahawa)* | 99,000,000 | 99,000,000 |
| | Wakulima(miche ya kahawa)* | 21,000,000 | 21,000,000 |
| | Tengo la mikopo mibaya | (38,790,456) | - |
| | Jumla ndogo | 105,907,560 | 125,235,576 |
| | Jumla Kuu | 169,021,018 | 172,550,549 |
| | *mkopo wa muda mrefu, marejesho yataanza baada ya miaka mitatu(3) | | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Jedwali Na.6 | Fedha Taslim na Benki | **31.03.2022 TSHS** | **31.03.2021 TSHS** |
| | Bank NMB PLC (Ofisi Kuu) | 850,104 | 5,338,398 |
| | NMB Bank PLC (coffee)30410006857 | 38,822,838 | 35,402,315 |
| | Tanzania Commercial Bank | - | 217,121,600 |
| | CRDB Benki (coffee)0150590775600 | 1,975,482 | - |
| | Jumla | 41,648,424 | 257,862,313 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Jedwali Na.7 | Akiba za kisheria | | |
| | Akiba ya lazima 20% | 3,263,066 | 3,263,066 |
| | Akiba ya Hisa | 2,447,300 | 2,447,300 |
| | Jumla | 5,710,366 | 5,710,366 |

| Jedwali za Taarifa za fedha kuishia tarehe 31 machi 2022 | | | |
|---|---|---|---|
| | | 31.03.2022<br>TZS | 31.03.2021<br>TZS |
| Jedwali Na.8 | Wadai wa muda Mrefu | | |
| | TADB | 403,695,386 | 440,000,000 |
| | Jumla | 403,695,386 | 440,000,000 |

**Maelezo ya ziada**

Tarehe 05 Juni 2020 WAMACU LTD tulisaini mkataba na benki ya kilimo TADB wenye wenye thamani ya Tshs 1,682,500,000 wenye sehemu mbili(2) kwa madhumuni yafuatayo;

SEHEMU 1

Sehemu ya 1 inahusu Tshs 1,000,000,000 kwa ajili ya kugharamia shughuli za ununuzi wa kahawa katika msimu 2020/2021. Pia Tshs 300,000,000 kwa ajili ya kuchukua deni la WAMACU wanalodaiwa na Benki ya NMB

SEHEMU 2

Tshs 262,500,000 kwa ajili ya kuongeza thamani zao la kahawa ikiwa ni pamoja na kutengeneza vitalu vya kuzalishia miche ya kahawa.

Mkopo huu unatolewa kwa awamu kulingana na mahitaji. Katika Msimu 2021/2022 Tshs 550,000,000 zilitolewa kwa ajili ya ukusanyaji Kahawa kwa riba ya 9%

| | | 31.03.2022 | 31.03.2021 |
|---|---|---|---|
| Jedwali Na.9 | Hesabu ya Wakulima | TZS | TZS |
| | Salio anzia | 123,215,263 | 39,234,540 |
| | Ziada ya mwaka huu | 77,860,192 | 83,980,722 |
| | Salio ishia | 201,075,455 | 123,215,263 |

| Jedwali za Taarifa za fedha kuishia tarehe 31 machi 2022 | | | |
|---|---|---|---|
| Jedwali Na.10 | **Wadai wengine** | 31.03.2022 TZS | 31.03.2021 TZS |
| | COASCO | 2,300,000 | 1,800,000 |
| | JK Mugendi | 3,859,375 | 3,859,375 |
| | Lukasi Maasa | 4,930,000 | 4,930,000 |
| | Wasaga Janja | 1,887,230 | 1,887,230 |
| | Wadai | 6,597,500 | 6,597,500 |
| | Acrrual Salaries | 3,650,000 | 3,650,000 |
| | Ushuru wa Halmashauri(mazao) | - | 70,522,627 |
| | Kema AMCOS | - | 31,525,313 |
| | Sirari AMCOS | 908,120 | - |
| | Wadai wengine | 1,961,578 | 1,961,578 |
| | Malipo ya pili Wakulima | 288,836 | 113,006,800 |
| | Jumla ndogo | 26,382,639 | 239,740,423 |
| | | | |
| Jedwali Na.11 | Ushuru wa Chama Kikuu | | |
| | kilo 177,109*60 | 10,626,540 | 17,730,300 |
| | | | |
| Jedwali Na.12 | Mapato Mengine | | |
| | Ukodishaji wa kiwanja-Nyamongo | 11,300,000 | |
| | Riba kutoka benki | 178,456 | |
| | Jumla | 11,478,456 | |
| | | | |
| Jedwali Na.13 | Gharama za watumishi | | |
| | Mishahara | 26,377,600 | 17,220,000 |
| | Vibarua | 388,450 | 7,659,750 |
| | Chakula na vinywaji | - | 1,108,500 |
| | NSSF | 3,348,000 | - |
| | Jumla | 30,114,050 | 25,988,250 |

| Jedwali za Taarifa za fedha kuishia tarehe 31 machi 2022 | | | |
|---|---|---|---|
| | | 31.03.2022<br>TZS | 31.03.2021<br>TZS |
| Jedwali Na.14 | Gharama za Utawala | | TZS |
| | Shajala | 2,900,800 | 936,500 |
| | Kodi ya zuio | 157,282 | - |
| | Stamp duty | - | 130,000 |
| | Mkutano Mkuu | 20,535,000 | 4,080,000 |
| | Usafi wa ofisi na mazingira | 2,149,100 | 821,000 |
| | Ada ya ukaguzi | 1,000,000 | 1,200,000 |
| | Sikuku ya wakulima | - | 765,158 |
| | Safari na posho | 3,680,000 | 12,889,000 |
| | Makaribisho | - | 629,055 |
| | Maandalizi ya makisio | - | 250,000 |
| | Matengenezo ya ofisi | 2,290,200 | 2,344,000 |
| | Elimu na semina | 1,320,000 | 1,610,000 |
| | Maji na Umeme | 28,000 | 180,000 |
| | Mawasiliano | 180,000 | 1,236,350 |
| | Vikao vya bodi na kamati | 10,087,800 | 3,430,000 |
| | Uchakavu | 1,800,000 | 1,001,250 |
| | Gharama za benki | 912,764 | 642,680 |
| | Uthamanishaji wa Mali (Ex-MCU) | 8,017,500 | - |
| | Matangazo na uhamasishaji | 6,775,000 | - |
| | Matayarisho barua pepe(website) | 1,640,000 | - |
| | Kiingilio TFC | 1,000,000 | - |
| | Kujali jamii (CSR) | 7,000,000 | - |
| | Bima ya majengo | 2,022,284 | - |
| | Tengo la Madeni mabaya | 38,790,457 | - |
| | Jumla | 112,286,186 | 32,144,993 |

| Jedwali za Taarifa za fedha kuishia tarehe 31 machi 2022 | | | |
|---|---|---|---|
| | | 2021/2022 | 2020/2021 |
| Jedwali Na.15 | Manunuzi/Malipo ya wakulima | TZS | TZS |
| | Muriba AMCOS | 14,448,000 | 28,753,600 |
| | Bungurere AMCOS | 24,041,600 | 43,792,000 |
| | Gorog'a AMCOS | 39,800,000 | 52,833,600 |
| | Nyantira AMCOS | - | 16,920,000 |
| | Itiryo AMCOS | 19,483,200 | 65,009,600 |
| | Kangariani AMCOS | 42,955,200 | 39,816,000 |
| | Maisome AMCOS | 8,524,570 | 16,614,400 |
| | Mbogi AMCOS | 16,360,000 | 6,676,800 |
| | Tagare AMCOS | 51,801,600 | 45,675,200 |
| | Nkongore AMCOS | 1,336,000 | 1,364,800 |
| | Nyamwigoma AMCOS | 4,510,400 | 1,683,200 |
| | Kema AMCOS | 41,528,000 | 56,056,000 |
| | Kemakorere AMCOS | 7,475,200 | 7,084,800 |
| | Sirari AMCOS | 908,120 | 15,294,400 |
| | Nyakonga Amcos | 9,236,800 | 5,596,800 |
| | Nyandurumo AMCOS | 6,542,400 | 2,948,800 |
| | Mwesu AMCOS | 1,174,400 | 1,214,400 |
| | Mogabiri AMCOS | 1,796,800 | 1,172,800 |
| | Mori AMCOS | - | 26,787,880 |
| | Jumla | 291,922,290 | 435,295,080 |

Jedwali Na.16 Hesabu ya Mazao

| MAPATO | JEDW | 2021/2022 TZS | 2020/2021 TZS |
|---|---|---|---|
| Mauzo ya kahawa | | 500,590,933 | 692,186,099 |
| **Toa: Gharama za Mauzo** | | | |
| Bidhaa mwanzoni | | 7,764,086 | 7,200,000 |
| Ongeza: Manunuzi | 15 | 291,922,290 | 435,295,080 |
| Gharama za Vibarua | | 2,011,600 | 787,100 |
| Kahawa kwa ajili ya kuuza | | 301,697,976 | 443,282,180 |
| Toa; Bidhaa mwishoni | 4 | 31,128,000 | 7,764,086 |
| Gharama za mauzo | | 270,569,976 | 435,518,094 |
| Faida ghafi | | 230,020,956 | 256,668,005 |
| **Toa: Matumizi** | | | |
| Usafirishaji wa kahawa | | 6,309,400 | 8,310,000 |
| Manunuzi ya magunia | | 8,775,000 | 10,252,000 |
| Ushuru wa Vyama vya Msingi | | 3,095,020 | 23,153,281 |
| Ushuru wa Chama Kikuu | | 10,626,540 | 17,730,300 |
| Ushuru Halmashauri ya Wilaya Tarime | | 2,694,816 | 8,191,320 |
| Ushuru Halmashauri ya Mji Tarime | | - | 102,870 |
| Ushuru H/shauri ya Wilaya Sengerema | | 311,520 | 311,520 |
| Riba ya mkopo benki | | - | 13,358,649 |
| Ada ya utafiti wa Kahara TACRI | | 1,865,915 | 2,595,845 |
| Ada ya mauzo ya Kahawa nje ya nchi | | 4,975,803 | 6,922,254 |
| Gharama za benki | | 1,538,881 | 2,500,520 |
| Shajala | | 1,276,600 | 1,106,000 |
| Kodi ya ghala | | 10,723,729 | 27,327,050 |
| Kusafirisha sampuli ya kahawa | | 55,000 | 60,000 |
| Matengenezo ya mizani | | 1,530,000 | 720,000 |
| Ada ya Wakala wa Vipimo | | - | 690,000 |
| Vibarua | | - | 564,084 |
| Gharama za mtunza ghala | | 22,791,524 | 11,667,090 |
| Gharama za ukoboaji | | 22,823,600 | 37,124,500 |
| Riba ya mkopo benki | | 52,767,416 | - |
| **Jumla ya matumizi** | | 152,160,765 | 172,687,283 |
| **Ziada(upungufu)** | | 77,860,192 | 83,980,722 |